

**Februari 2017**



Wapendwa marafiki,

Kwa miaka mingi, nimeshauri wanandoa wengi wanaotafuta ushauri na maombi kwa ajili ya ndoa na familia zao. Nimegundua kuwa ndoa nyingi zina matatizo mengi na maneno machache tu ya kuwatia moyo yanakuwa kama maji baridi, yanayoponya ndoa zilizokaukiwa na kuvunjika.

Tunaposonga mbele na mabadiliko yetu ya kuwa Wanawake wa matumaini wa TWR, tambua kuwa alama yetu mpya inaonyesha jinsi mioyo yetu inavyounganika na wenzetu wengine kisha na Mungu pia. Kwenye Ezekieli 36:26, tunamsikia nabii akituambia kuwa Mungu ataiondoa “mioyo yetu ya mawe” na kutupa “mioyo mipya.”

Kwenye ndoa wakati mwingine, tunaweza kujisikia kama tuna mioyo ya mawe kila mtu kwa mwenzake. Ndoa nzuri hugharimu muda na usikivu. Kuna vita kwenye ndoa yako ambayo si ya ulimwengu huu. Mara nyingi tunapokutana na majaribu kwenye ndoa zetu, tunaanza kujisikia kuwa wenzi wetu ndio adui zetu. Hata hivyo yupo adui halisi, naye ni mwenzi wako wala watoto wako.

Na utiwe moyo leo kuwa haupo peke yako kwenye changamoto unayokabiliana nayo kwenye ndoa yako.

Utiwe moyo kuwa Mungu anajua hali unayoipitia na yuko hapo kukusaidia.

Mazingira sio rahisi sana, lakini Mungu hayupo mbali sana kuwa ngome yako na msaada nyakati za shida na unapomhitaji. (Zaburi 46:1).

Usikate tamaa kuipigania ndoa yako. Endelea kuomba pamoja na wanawake wengine na kumuinulia, Mungu changamoto na magumu uliyonayo. Mkabidhi maumivu na hasira, uchungu na ugumu wa kusamehe. Amini kuwa yupo Mungu anayekupenda na anayeweza kuona yale unayoyapitia. Uwe jasiri na uwaeleze wenzako kwenye kikundi cha maombi changamoto unazokabiliana nazo, kisha zipeleke kwa Mungu kwa njia ya maombi ukiamini kuwa anasikia maombi yetu na yupo karibu nao waliovunjika mioyo. (Zaburi 34:18). Tembea ukiwa huru pasipo kushikilia uchungu au hasira, na mruhusu Mungu aiendeshe ndoa na familia yako.

Tunaweza kudumu katika maombi. Tunaweza kushikana mikono tunapomlilia Mungu kwa ajili ya ndoa na familia zetu, tukiamini kuwa tunamtumikia Mungu anayetamani ndoa na familia zetu zilete utukufu kwa Jina lake ili wengine waweze kumjua Yesu.

Usikate tamaa! Elekeza macho yako kwa Yesu; yeye yupo kwa ajili yako wewe pamoja na ndoa yako. Ninakuomba leo hii!

Katika yeye mioyo yetu inashangulia,

**Peggy Banks**

Mkurugenzi wa Kimataifa

TWR Women of Hope/Project Hannah